



CHUSOMENI

KIBAJUNI

KIVANGO 2

Yumna Hamid Titi

Fuad Aroi

Yumbe Athman

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.

Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi

Mpesi Lane

S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya

Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740

Barua pepe: info@twawezacommunications.org

Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nda Twaweza Communications

Chapisho la Kwanda 2024

ISBN: 978-9966-128-17-1

Kitabu cha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha utamaduni wa Vabajuni. Nradi huu huṭekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na UK's Department for Culture, Media and Sport.



Aliomo

1: Sukuli	1
2: Sukuli	8
3: Vaṇama Va Kuewa.	13
4: Usafi	18
5: Usalama	23

SHUKURANI

Dhiṭabu dha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṭamaduni wa Vabajuni. Chwaṭoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuandika na kuchapisha dhiṭabu hidhi. Bila nsaada wavo ingalikuva ṭabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a kuifundrisha kusoma na kuandika Kibajuni. Chwavashukuru Dkt. Rukiya Harith na Nafisa Awadh kwa ushirikiano wavo na vaandisi kachika haṭua dhoṭe dha kuandika nfulululidho wa *Chusomeni Kibajuni*. Vaandisi va dhiṭabu hidhi –

Yumna Hamid Titi, Fuad Aroi na Yumbe Athman – valiṭolea kushiriki na kumalidha kuandika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia chwanshukuru Athman Tora (Lalavani) na vale voṭe chufanyao navo kadhi hii adhwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṭamaduni wa Vabajuni.


Kimani Njogu, Twaweza Communications
Omar Lali, Shungwaya Welfare Association
Athman Lali Omar, Swahili Resource Centre

Juni, 2024


Kusikidha

Kuandama maagidho

A



B



C



D



Asikidhe maagidho a mwalimu.

Kudhungumudha

Kutoa maagidho



Wimbo wa kuuka kamba

Kibibi watokapi?

Mambasa,

Kunani?

Si kichu,

Haya kwaheri,

Ṭinda kuku,

Kuku, ṭinda baṭa,

Bata, ṭinda kuku



Kuku ṭinda baṭa.

Kadhi a dhikundri

Kachika makundri, vanafunḡi vaṭabe shuhuli mbalimbali dha darasani.

Kusoma


Kusoma michoro



Maagidho

1. Ilenge michoro hii na ueledhe uvonacho.
2. Chungu senchensi ukichumia michoro hii.

Kusoma kifungu



Soma kifungu hichi na ujibu maswali

Midhe ndhivu

Sukuli a Kaa chonjo ni nduri sana. Vanafundi na valimu vote vana biḡii. Midhe nae husoma kachika sukuli hio. Lakushangadha ni kuva Midhe ni nkulivu. Kila siku iye hungia sukuli akiva mechelewa. Vanafundi ndrudhe na valimu vandojaribu kila ndia kumuekedha lakini Midhe ndokuva ishikio la kufa halisikii dawa.

Siku moya Midhe aliambiwa arudi nmbani aye na ndhadhi wake. Midhe aliposikilia kwavo alindhulia mwalimu kuva unchukanie inya na ishe. Ishe alipandwa na mori akaya sukuli utukudhie bakora kutaka kumpondra mwalimu.

Mwalimu alimpodha akamueledha dhichendro dha mwanawe. Ishe akapoa mocho. Midhe akaambiwa aeche mabuku ake. Mwalimu akanvonesha ishe kadhi ambadho Midhe hafanyi. Ishe akayiva kuva mwanawe ni ndhivu.


Midhe alikanywa na ishe. Aliyuti na kuomba nsamaha kuva hatarudia tena.

Masuali

1. Midhe husoma sukuli gani?
2. Ishe Midhe alitukua nini alipokwendra sukuli?
3. Chaya tabia mbili dha Midhe?,
4. Je, tabia ulidhodhichaya dha Midhe ni nduri?
5. Ishikio la kufa
6. Hadisi hii indochufundrisha nini?

Kuandika

Kuandika maina a dhichu dha sukuli



Maagidho

1. Andika maina a dhichu uvonadho kwenye nchoro.
2. Chumia maina hao uchunge senchensi.

Kuandika

Harufu kuru na ndrodi

Andika senchensi dhifuachadho kwa harufu kuru

Nfano: sukuli a siyu husifika..

SUKULI A SIYU HUSIFIKA.

1. Mwalimu aliandika ubavoni.

.....

2. Sukuli echu ina uvanda nkuru.

.....

3. 3.Mwanafundi hodari hupawa dhawadi.

.....

Andika senchensi dhifuachadho kwa harufu ndrodi.

Nfano: KİTABU KİKO YIU A MEDHA.

Kiṭabu kiko iyu a medha.

1. I.KALAMU ANGU INDOPOṬEA.

.....

2. MWALIMU HUSOMESHA KWA UDHURI.



.....

3. MABUKU ALIRARUKA.

.....

Kusikidha

Kuandama maagidho



Eledha uvonacho.

Kudhungumudha

Dhichandrawili/ dhichondrovi

Tauwa dhichandrawili/dhichondrovi dhifuachadho

1. Pa! Pa! Mpaka nsikichini.
2. Kitam tamu mivani.
3. Chandrika kichanga chule kunadhi.
4. Papo sikivoni.
5. Asikari nlangoni.
6. Vadhungu vavili hutungia idirishani.
7. Huendra na namba angu.
8. Vanangu hucheche ntana, usiku hupachana.
9. Kibibi hupepecha npunga.
10. Hutembea iyu a miva lakini hainichofi.

(kufuli, kishogo, kope, kamasi, kiachu, ulimi na menyo, nocha angani, nlango, kichakwi, fududu/kobe)

Kusoma


Kusoma senchensi

Soma senchensi dhifuachadho

1. Jamuhuri ni mwanafundi mwenye bidii.
2. Amani hufanya matedho darasani.
3. Vanafundi hutedha uvandani.
4. Sukuli echu ina matokeo madhuri.
5. Medha a mwalimu indovundika.
6. Michi a sukuli ilikauka.

Kusoma

Kusoma kifungu



Siku a dhawadi sikuli

Vadhee valinena kijaa chema huveshwa peche. Siku a kila nchu kuvuna alichopandra ilisikilia. Vageni, vadhadhi, valimu na vanafundi valiyaa kwenye ukumbi wa sukuli echu.

Vanafundi ambavo valifanya udhuri kachika mitihani avo valikuva vameyawa na furaha. Kwa upandre nngine vatee valivokosa alama nduri valiyawa na jitimai.

Mwalimu alisimama akavakaribisha vadhadhi na vageni. Pia alivachia moyo vanafundi vote kwa kuvaambia kuwa kuna dhawadi dha kila aina. Alinena kuna dhawadi dha alama nduri, dhawadi dha mwanafundi mwenye adabu nduri na

dhawadi dha mwanafundi nsafi. Amina alisikia raha sana kwa kuwa iye hashiki kichu darasani lakini kila siku huwa mwanafundi wa kwanda kusikilia sukuli.

Wakati wa dhawadi uliposikilia, vanafundi vakapawa dhawadi dhavo, vakafurahi sana. Ndhadhi wa Amina nae aliterema nno kwa kuwa mwanae ndopacha dhawadi. Alinena kuwa Mungu ni nkuru hakupoki ote.

Vanafundi valibika kusi. Vachu vote valifurahi na vakarudi majumbani kwavo kwa furaha, kuterema na dhigelegele.



Jibu masuali

1. Vachu valikusanyika kwa shuhuli gani?
.....
2. Ni vanafundi vapi valiyawa na furaha?
.....
3. Ni vanafundi wa aina gani valipacha dhawadi?
.....,,
4. Amina alipawa dhawadi kwa sababu gani?
.....
5. Kijaa chema huvishwa
.....

Kuandika

Kuandika senchensi

Andika senchensi kulingana na michoro hii.



Kuandika

Kuandika senchensi


Panga maneno uundre senchensi sahihi

1. nchafu barikoa ni mwana.
2. nkuru uvanda wechu ni.
3. kwendra kengele indolia a nmbani.
4. angu rafiki mwerevu ni.
5. michi ndarandara chusikache.


Kusikidha

Nganu a vaṇama va kuewa


A




B



C



D



Masuali

1. Nganu a mwalimu ilihusu nini?

.....

2. Mwalimu andovachaya vaṇama gani?

.....


3. Undoifundra nini kutokamana na nganu?

.....


Kudhungumudha

Chaya dhichu dhilidhoko kachika michoro.

A




B



C



D



Maagidho

Kadhungumudhe na vachu va ħumbani kuhusu faida a vaḡama va kuenta.

Ufahamu

Alitoka nchu kae na majumba na matae, taratara simambae, taka la wisha ama la bakae?

Hapo dhamani dha kae vanama vote valikuva vakiishi mwichuni. Ikatokea siku moya vakadirikana kula shauri baada a kuvona chaka kimedhidi. Vanama valikuva vakiliwa na simba.

Kachika nkuchano wavo, kuna valoamua kwendra muini kufanya kadhi ili vapache chakula. Ng'ombe na mbudhi vataadhanya idhiva, pundra na ngamia vatakuva makwiji va midhigo, imbwa atalindra, hondoo atadhanya manyoa na paka atashika pana.


Valiposikilia n'yini, pana alivachangadhia vachu kuva hava vanama valokuya muini vana nama tamu sana. Vachu vakaanda kuvatinda vanama havo. Hili lalinfanya pana kufurahi kusalia mekoni kungoja dhinofu dhishopoke.

Jibu masuali

1. Vanama valikuva vakiishi kwapi?
.....
2. Kwa nini valikula shauri?
.....
3. Mbudhi na ng'ombe valiamua kufanya nini?
.....
4. Pundra na ngamia vatakuva nyani?
.....
5. Faida a paka ni ipi?
.....

Kuandika

Chaya harufu dhilidhoko kwenye ishambu la maneno



Maagidho

Andika maneno haa kwa hati nduri.

1. Ng'ondra
2. Ng'ombe
3. Pundra
4. Farasi
5. Idhiva
6. Ngodhi
7. Wisha
8. Nama

Kuandika

Yadha pengo dha maneno haa

1. U_an_a
2. F_ra__
3. Ng'_m_e
4. Ho_d_o
5. Mbu__i
6. K_k__
7. I_ita
8. P_k__
9. Im__a
10. __amia

Kusikidha

Ufahamu

Chufundrishane usafi

Usafi ni yambo muhimu kachika maisha a binadamu. Madhingira a binadamu ni muhimu kuva safi, haswa madhingira a numbani na binadamu mwenewe.

Nchu hufaa kuandaa kwa usafi wa nvili wake. Ili kuva nsafi wa nvili, nchu hufaa kukoa, kuvaa nguvo safi, kukacha madowe, kutana nee na mangingeo.

Usafi ukidumishwa maradhi hupungua na nchu huva na afia nduri. Usafi wa numbani pia ni muhimu. Kila mwana hufaa kuhakikisha numbani kwavo ni kusafi, haswa chumbani ayalapo.

Uchafu wa chaka ukusanywe na kuwedha kuchiwa mocho na dhingine hata kukusanywa na kuvekwa sehemu mbali kama dhile dhipandre dha dhijaya na misumari.

Usafi ni yambo muhimu sana kwenye maisha echu. Vilevile chuwedhe kudhingatia usafi hata sukuli. Sehemu a chooni chuveni na tahadhari kwani ndripo uchafu mwingi hupachikana. Vana vote vatakiwa kudhingatia usafi.

Jibu masuali

1. Pahali popote chuishipo patakiwa kuveye?
2. Ni mambo gani yadhungumudhwao kwene aya a kwanda?
.....
3. Hufaa kufanya nini kuiyepusa na maradhi?
4. Chaya sehemu chachu dha kudhingatia usafi,
.....,
5. Chaya kitwa cha kifungu hichi

Kudhungumudha

Madhungumudho kuhusu usafi

- Radhia:** Huyambo ndruangu?
- Salama:** Siyambo mwenechu.
- Radhia:** Vadhadi vako vakeeye?
- Salama:** Havana neno na vako navo?
- Radhia:** Vote vadhima.
- Salama:** Mwenechu mbona nee ni ichowe?
- Radhia:** Imi sina haja a kutana wala kukota.
- Salama:** Usafi ni yambo muhimu.
- Radhia:** Usafi ni kutana nee tu?
- Salama:** Hata madowe ako ni makuru.
- Radhia:** Mwenechu chuate madhungumudho hao.
- Salama:** Ndruangu ladhima nikwambie.
- Radhia:** Enhee.
- Salama:** Ladhima ukoe na kubika nsuaki kila siku.
- Radhia:** Kuandia eo nami takuwa nsafi.
- Salama:** Ndrio mwenechu. Chudhingatie usafi.

Jibu masuali kulingana na madhungumudho haa

1. Madhungumudho haa ni kuhusu nini?
.....
2. Madhungumudho haa ni kachi a nyani na nyani?
.....
3. Radhia alikuva ni mwana gani?
.....
4. Madowe a nyani alikuva makuru?
.....
5. Je, Salama alikuva rafiki ndhuri?
Kwa nini?.....

Kusoma

Ushairi

Vana va chumba cha pili, ni vasafi va kisasa
Huisafisha kikweli, si mambo a kupapasa
Na hachuna mushikili, usafi hushindra pesa
Usafi yambo muhimu, kwa wingi chudumisheni
Usafi haswa numbani, na wa nvilini pia
Chusafishe mabandrani, mahali pa kukejia
Usafi chudumisheni, haswa sukuli sikia
Usafi yambo muhimu, kwa wingi chudumisheni
Kukoa ni namba wani, mai nchu kuichia
Akalowa nvilini, sabuni a kunukia
Na nsuaki menyoni, ladhima kuibikia
Usafi yambo muhimu, kwa wingi chudumisheni

Usafi wangu mwenewe, nieledhe avelee
Ni usafi wa madowe, pia usafi wa nee
Usikubali michove, mitava ikuenee
Usafi yambo muhimu, kwa wingi chudumisheni

Kusoma

Soma senchensi hidhi

1. Ni muhimu kuveka madhingira echu safi.
2. Michi ina manufaa mangi kachika maisha echu.
3. Nvili nchafu huecha maradhi.
4. Chaka dhote dhichiwe kwenye mapipa a chakachaka.
5. Vanafundi vasome kwenye madarasa safi.
6. Choo ladhima kive safi.

Kuandika

Haṭi

Andika senchensi hidhi kwa haṭi nduri

1. Napenda kukoa kivilivili changu.
2. Numbani kwechu ni kusafi.
3. Imi hupenda kuveka madowe mafupi.
4. Nee hutakiwa kutanwa au kukotwa.
5. Maradhi mangi husababishwa na uchafu.

Kuandika

A. Kuunganisha silabi



1. Ma-ra-dhi
2. Cho-o
3. Ma-dhi-ngi-ra
4. Ku-ku-sa-nywa.....
5. Ki-pi-ndru-pi-ndru

B. Panga harufu hidhi upache ineno sahihi

1. nibusa
2. takoku
3. chafuma
4. kinasu
5. tanaki.....


Kusikidha

Kusikidha maagidho



Kachika dhikundri jadilianani mbinu dha kudhivia ajali.

Kusimulia dhisa



Enga picha na ueledhe uvonacho.

Mueledhe mwendaako kisa kuhusu ajali iliotokea kijijini kwenyu

.

Wimbo



Ngoma mwangoma, ngoma.
Kidhere changu cha kae, ngoma.
Hunipi nami wasia, ngoma.
Na wasia nikupao, ngoma.
Kivona dhicha kimbia, ngoma.
Kitwa chia ishakani, ngoma.
Maguu ekedha ndia, ngoma.
Adui akipicha, ngoma.
Tanena umeifia, ngoma.
Ngoma mwangoma, ngoma.

Siifanye nshindrani, ngoma.
Ajali haikujali, ngoma.
Tukua na tahadhari, ngoma.
Usiichie kiburi, ngoma.

Panga chumia hondreni, ngoma.
Kisu kichie uvoni, ngoma.
Mocho udhinye mekoni, ngoma.
Wendrapo matembedhini, ngoma.
Ngoma mwangoma, ngoma.

Kusoma

Hadisi/Nganu

Ajali haijali



Chukiva numbani ajali hutokea dha kila aina. Ajali hadhitau
nchu wala wakati. Hutokea bila kutarajiwa. Kuna ajali dha
kila aina, kwa nfano: Mocho, kuitinda kwa kisu, kuumwa na
vadudu, kuchekechea kwa mai mocho na ngingi ninginedho.

Ingava huneneka kuva ajali haina kinga, lakini ladhima chuiṭahadhari. Chwaṭakiwa kuva makini mekoni, dhisu dhenḡ makali, dhivekwe mbali na vana dhidodi. Chusiṭe mocho uvake wakaṭi hachupiki dhakula. Vana vasiṭwe kuṭedhea mocho na mai akisuka iṭi afuchwe asimuanguse nchu.


Maeneo chuishio ave safi. Chusiṭe magugu kumea kuva marefu. Magugu marefu husiṭa vadudu haṭari. Ṭupa dha kuvundika zisiṭwe kuenea kila pahali na dhijaya dhidhikwe nṭangani. Usiṭe kibahalulu karibu na kichandra au padhia, huwedha kusababisha mocho.

Jibu masuali

1. Chaya ajali chachu dhiṭokeadho ṇumbani.
.....
2. Chukiva mekoni chwaṭakiwa kuvae?
.....
3. Dhijaya dha ṭupa dhivekwe kwapi?
.....
4. Ni nini ilosababisha mocho kwenḡ nchoro?
.....
5. Chaya kiṭwa cha hadisi hii?
.....

Kuandika

Kuandika senchensi



Ukiva na mwendako andika senchensi mbili kwa kila nchoro.

Kuandika

Kupanga senchensi

Panga senchensi upache kifungu sahihi

1. Alijepa kisu mekoni.
2. Dakitari alimfunga bendreji.
3. Asha ni nkaidi.
4. Akaikacha kijaa.
5. Akarudi numbani.
6. Alipekwa sipichali.

Nfano:

1. Asha ni nkaidi
- 2.
- 3.
- 4.
- 5.
- 6.